**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA

*Unapojibu Tafadhali taja:*

**Kumb. Na.MODC/A.10/38/74** **31 May, 2021**

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (MARUDIO)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika nafasi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na Tangazo hili linatokana na Kibali cha Ajira mbadala kilichotolewa kwa barua yenye Kumb. Na: FA.170/571/01/``A``/05 ya tarehe 08 Februari 2021, kutoka kwa Katibu Mkuu OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### I. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III – Nafasi 01.

**SIFA ZA MWOMBAJI;**

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
2. Awe amehitimu mafunzo katika ngazi ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI/ MAJUKUMU**

I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
V. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika kijiji.
VI. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
VII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
IX. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
X. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

*Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), **Chitete - MOMBA**, S. L. P. 273, TUNDUMA –MOMBA-SONGWE.*

Baruapepe: ded@mombadc.go.tz Tovuti: www.mombadc.go.tz

XI. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**Mshahara;**

Ngazi ya Mshahara wa Serikali **TGS B**.

1. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Ijumaa,tarehe 14 June 2021,saa 09:30 Alasiri.
2. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Momba,
S.L.P. 273,
**TUNDUMA-MOMBA**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MOMBA DISTRICT COUNCIL
MOMBA

Adrian J.Jungu
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA**

**Nakala:** Katibu Tawala (M),
S.L.P 23
**SONGWE.**

Katibu Tawala (W),
S.L.273,
**TUNDUMA-MOMBA.**

Mbao zote za Matangazo,
Kata zote
Halmashauri ya Wilaya ya Momba,Tunduma Mji.